Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU *Bulletin*

*JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.32 - 2023*

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023

# Sasa Rasmi



# Miaka 50 ya Mafanikio ya NECTA

## Serikali kuimarisha mikakati ya kupunguza udanganyifu mitihani

**- KAZI IENDELEE -**



## BODI YA UHARIRI

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
*Kamishna wa Elimu*

Atupele Mwambene
*Mkurugenzi wa Sera na Mipango*

Sylvia Lupembe
*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini*

Nelly Mtema
*Mhariri Msaidizi na Mwandishi TSN*

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Ipyana Mwaipaja
Veronica Chitunda

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## SERIKALI KUENDELEA KUIJENGEA UWEZO NECTA KUMUDU MABADILIKO YA TEKNOLOJIA

Disemba 16 2023 Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) liliadhimisha Miaka 50 tangu lilipoanzishwa Novemba 21, mnamo mwaka 1973. Tuna kila sababu ya kujivunia kazi nzuri iliyofanywa na NECTA kwa kipindhi cha 50 katika kusimamia mitihani kwa weledi mkubwa na kuisaidia serikali kuchuja na kufahamu umahiri wa wanafunzi.

Katika kuthamini umuhimu na kazi kubwa iliyofanywa na Baraza hilo, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan alizindua mnara wa kumbukumbu ya Maadhimisho hayo, ambayo yaliongozwa na kauli mbiu inayosema "Upimaji wa Umahiri kwa Misingi ya Haki Suluhisho la Ajira Karne ya 21"

Kupitia Maadhimisho hayo Rais Samia aliitaka NECTA kuongeza umakini katika utungaji, usahihishaji na udhibiti wa mitihani na kuondoa mianya yote inayoweza kuruhusu wahitimu wasiokuwa na sifa ili kuisaidia Serikali kufikia malengo ya upimaji unaozingatia haki na hatimaye kuwezesha upatikanaji wa nguvu kazi sahihi itakayoshiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa.

Pia aliiagiza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kushirikiana na Baraza hilo kuwa na mkakati wa kushughulikia changamoto ya udanganyifu wa mitihani.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema katika kipindi cha miaka 50, NECTA imekuwa chujio la kuwapata wanaostahili kwenda kwenye ngazi za juu na hata kulitumikia Taifa kupitia ajira zinazotolewa na Serikali, ambapo mafanikio hayo yametokana na jitihada mbalimbali zilizofanywa na Kamati za Mitihani za Mikoa na Wilaya ambazo zimesaidia kudhibiti kikamilifu wizi wa mitihani.

Rais Samia alisema serikali itaendelea kuijengea uwezo NECTA na walimu ili kuhakikisha ufundishaji, usomeshaji na utahini unafanyika kwa umahiri mkubwa kuwezesha watahiniwa kumudu mahitaji ya mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

Tunaipongeza serikali kwa kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya elimu ikiwemo vifaa vya TEHAMA ambavyo vimeimarisha utendaji wa Baraza na kuongeza matumizi ya teknolojia katika usajili wa watahiniwa, uchapaji na usahihishaji wa mitihani pamoja na uchakataji wa matokeo.



Uhitimu mahiri na Uadilifu >



# Miaka 50 ya Mafanikio ya NECTA Serikali kuimarisha mikakati ya kupunguza udanganyifu mitihani

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda ameitaka jamii kushiriki katika kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika vipindi vya mitihani, ili kulinda heshima ya elimu na Taifa kwa ujumla.

Prof. Mkenda alitoa rai hiyo jijini Dar es Salaam wakati akizungumza katika Ufunguzi wa Maadhimisho ya Miaka 50 ya Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) ambapo amesema wizi wa mitihani unaharibu maadili ya watoto na heshima ya taifa.

"Wizi wa mitihani si haki, naomba wananchi tushirikiane na Serikali kupiga vita vitendo vya udanganyifu, tudumishe uadilifu na kuwa wazalendo kujenga Taifa letu" alisema Prof. Mkenda.

Aidha Waziri Mkenda amelipongeza Baraza hilo kuendelea kusimamia kwa umahiri shughuli mbalimbali za Mitihani kwa kuzingatia sheria, sera na taratibu zilizowekwa, na kwamba hivi sasa limesaidia kukabiliana na changamoto ya udanganyifu katika Mitihani.

"Tuna kila sababu ya kujivunia kazi nzuri sana iliyofanywa na Baraza hili kwa Miaka 50 imesimamia mitihani kwa weledi mkubwa na limeisaidia serikali kuchuja na kufahamu umahiri wa wanafunzi" alibainisha Waziri Mkenda.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) Dkt. Said Mohamed amesema katika kuadhimisha Miaka 50, Baraza hilo limekutana na Wadau wa Elimu, kutathimini mafanikio, changamoto na kuweka maono kwa miaka ijayo kuendelea kuboresha utendaji kazi.

"Baraza limefanikiwa kwa ufanisi mkubwa kuendesha Kongamano la kitaaluma katika Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Wanataaluma kutoka sehemu mbalimbali nchini na wengine kutoka ng'ambo wameshiriki katika Kongamano hilo" alibainisha Dkt. Mohamed.

Aidha ameeleza kuwa Baraza pia liliendesha mafunzo kwa walimu wanataalum kuhusu namna bora ya kuandaa maswali ya umahiri.

Akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mkuu wa Wilaya ya Ubungo Mhe. Hashimu Komba amemshukuru Rais Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuboresha miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari kwa mkoa huo na sehemu nyingine nchini.

"Sisi tunajivunia mafanikio ya Baraza hili hasa katika kutekeleza majukumu yake kwa weledi, tutaendelea kushirikiana na NECTA kudhibiti vitendo vya udanganyifu katika Mitihani" alisema Ndug. Hashimu.

Nae Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Mitihani (NECTA) Dkt. Hassan Ally amesema mafanikio ya Maadhimisho hayo yanachangiwa na Usimamizi bora wa Wizara ya elimu inayohakikisha Taasisi zilizochini yake zinatekeleza wajibu wake kikamilifu kutimiza azma ya Serikali katika Sekta hiyo inafikiwa na kupata matokeo chanya.



Uwekezaji katika Sayansi>

# Mhe. Kipanga asisitiza kuwekeza katika sayansi, Teknolojia na uvumbuzi

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omar Kipanga amesema serikali imeendelea kufanya uwekezaji wa kutosha katika Taasisi za Elimu ya Juu nyanja ya tehama ili kusaidia kuzalisha wataalam wengi na mahiri watakaosaidia maendeleo ya uchumi wa kidigitali.

Mhe. Kipanga alitoa kauli hiyo jijini Arusha wakati akifungua Maadhimisho ya Miaka 6 ya Kituo cha Umahiri katika TEHAMA katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NM-AIST), ambapo amesema kuwa ustawi wa baadaye wa uchumi wa Afrika utaamuliwa na kiwango cha uwekezaji katika sayansi, teknolojia na uvumbuzi.

''Suala la ubunifu litaendelea kuwa muhimu na kuwa mstari wa mbele katika ukuaji wa uchumi kupitia sekta mbalimbali ikiwemo kilimo, usafirishaji, elimu na biashara. Katika miungo ijayo uwezo wa uvumbuzi ni muhimu kwa ajili ya ushindani kitaifa, kikanda na kimataifa" alisema Mhe. Kipanga.

Aidha ameishukuru seriakali ya Ujerumani, kupitia Taasisi yake ya GIZ pamoja na DAAD kwa kufadhili mradi unaolenga kuwajengea uwezo wanafunzi wa eneo la Afrika Mashariki katika Masuala ya TEHAMA.

''Program hii inajikita zaidi kwenye masuala ya TEHAMA, na mnafahamu hivi sasa ulimwengu unapoelekea, tunasema dunia ipo kiganjani bila kuwafunza vijana wetu umahiri wa eneo la hili tutaendelea kubaki nyuma" alieleza Mhe. Kipanga.

Ameongeza kuwa serikali ya awamu chini ya Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan imewajibika kikamilifu katika kufanya uwekezaji mkubwa kwanza kwenye miundombinu, kusomesha wataalam mbalimbali lakini pia katika kuhakikisha inaandaa bajeti ambayo itawezesha masuala ya tehama kufanyika kwa ufanisi.

''Katika Mwaka wa fedha 2023/24 serikali imetenga zaidi ya Bilioni 9 kwa ajili ya kuwezesha bunifu mbalimbali pamoja na teknolojia mbalimbali zilizoibuliwa ili ziende kuwa bidaa zitakazosaidia kutatua changamoto zinazokabili jamii yetu" alibainisha Mhe. Kipanga.

Nae Makamu Mkuu wa Taasisi ya Afrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia Prof. Maulilio Kipanyula amesema tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Umahiri katika Tehama wameweza kuzalisha wahitimu 136 kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Prof. Kipanyula amesema kuwa kituo hicho kinajivunia mafanikio makubwa ikiwa ni pamoja na kutoa ufadhili kwa Wanafunzi wote nchi za Afrika Mashariki kusoma katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela.

''Kama mnavyofahamu duniani kote tunazungumzia uchumi wa kidigitali, kazi yetu kubwa ni kuzalisha wanaafrika wenye uwezo wa teknolojia za kidigitali, ili kusukuma maendeleo ya kiuchumi na kuiwezesha Afrika Mashariki ishiriki kikamilifu katika uchumi wa kidigitali" alieleza Prof. Kipanyula.

Akizungumza kuhusu matarajio ya ufadhili kupitia kituo hicho Mwakilishi wa Taasisi ya DAAD ya nchini Ujerumani Bettina Onyango amesema taasisi inajivunia kuona kituo hicho kimefanikiwa kuanzisha program za shahada za Uzamili, na tayari kimezalisha wahitimu ambao ndio wanufaika kutoka nchi zote za Afrika Mashariki."

Ameeleza kuwa serikali ya Ujerumani inalenga kukuza maendeleo ya wanataaluma katika Vyuo Vikuu ili kuongeza umahiri na kuchochea maendeleo katika sekta mbalimbali za uzalishaji.



Utatuzi Changamoto >



# Watafiti Vyuo Vikuu watakiwa kutatua changamoto katika Jamii



Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amewataka watafiti katika Vyuo Vikuu nchini kutambua kuwa wanawajibu wa kutatua changamoto zilizopo katika jamii.

Katibu Mkuu amesema hayo wakati akifungua zoezi la utoaji wa zawadi kwa Wanachuo, Watafiti na Viongozi wa Chuo waliofanya vizuri kwenye masomo katika Ndaki mbalimbali za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Prof. Nombo amesema Chuo ni sawa na Kiwanda kama Hayati Mwalimu Julius Nyerere alivyosema, Chuo ni kama Kiwanda kwa sababu kinazalisha wataalamu wanaopaswa kutumia utaalamu wao kwa manufaa ya jamii hivyo kuonesha umaana wa elimu.

Alisema majukumu ya Vyuo Vikuu ni kufundisha, kutoa mafunzo, kufanya tafiti na kuzifikia jamii na kwamba kwa kupitia matokeo ya tafiti ndipo jamii itafikiwa kwa kutumia matokeo ya tafiti hizo kutatua changamoto zilizopo katika jamii.

Naye mmoja wa watafiti aliyepata tuzo ya mtafiti bora wa mwaka kutoka Kampasi ya Tiba ya Wanyama na Sayansi Afya, Profesa Robinson Mdegela amesema amefanikiwa kupata tuzo hiyo baada ya kufanya tafiti yenye kugusa maisha ya Watanzania ikiwemo kupambana na ongezeko la usugu wa vimelea vya magonjwa dhidi ya dawa tatizo linalokaribia kuua watu karibu 12500 kwa mwaka kiwango ambacho ni karibu mara 10 ya idadi inayosababishwa na malaria au UKIMWI.

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Prof. Raphael Chibunda amesema kwa mwaka huu 2023 wamefanikiwa kutoa zawadi 248. Tuzo hizi hutolewa kila Mwaka ili kuweka ushindani unaochagiza mabadiliko chanya

Prof. Chibunda amesema mabinti wanaonekana kuwa mstari wa mbele katika kupata zawadi na kuongezeka kila mwaka jambo ambalo linaashiria wanazidi kuongeza juhudi ya kusoma na kuweka changamoto kubwa kwa wanafunzi wa jinsia ya kiume.

Naye mwanafunzi aliyepata tuzo tatu ikiwemo ya mwanafunzi bora wa kike na pia mwanafunzi bora mwaka wa tatu kwa Shahada ya Usimamizi wa Nyuki na Rasilimali zake Vaileth Chiwango alisema atatumia tuzo hizo kubadilisha jamii hasa inayofanya ufugaji wa nyuki kizamani kwa kuwawezesha kutumia mizinga ya kisasa na kusimama ufugaji kimaendeleo.

Uimarishaji Elimu >

# Tanzania, Sweden zasaini mkataba msaada wa takribani bilioni 210 kuimarisha kada ya ualimu kupitia GPE

Tanzania na Sweden, kupitia Taasisi ya Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE) na Shirika la Kimataifa la Ushirikiano wa Kimaendeleo la Sweden (SIDA), zimesaini Mkataba wa msaada wenye thamani ya dola za Marekani milioni 84 sawa na takriban shilingi bilioni 210, kwa ajili ya kuimarisha utekelezaji wa Programu ya kuimarisha Kada ya Ualimu nchini.

Mkataba huo umetiwa saini Jijini Dar es Salaam Katibu Mkuu Wizara ya Fedha Dkt. Natu El-Maamry Mwamba na Balozi wa Sweden nchini, Mhe. Charlotta Ozaki Marcias.

Akizungumza katika hafla hiyo Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. James Mdoe amesema ufadhili huo umekuja katika kipindi muafaka ambapo serikali imeboresha Mitaala ya ualimu hivyo utatumika kama ilivyopangwa kuimarisha utendaji wa walimu kuanzia mwaka 2023/24 hadi 2026/27.

Aidha ameongeza kuwa serikali imetekeleza kwa mafanikio miradi kupitia ufadhili wa awali wa GPE wa dola za Marekani milioni 225 sawa na takriban shilingi bilioni 562 zilizotumika kugharamia utekelezaji wa programu ya kuimarisha stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu awamu ya kwanza kuanzia 2013 - 2018 na awamu ya pili inayoishia 2024.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha ambae pia ni Mlipaji Mkuu wa Serikali Dkt. Mwamba alisema kuwa Mkataba huo utaongeza jumla ya misaada kutoka GPE nchini Tanzania kufikia dola za Marekani milioni 309, sawa na takriban shilingi bilioni 773 na kwamba fedha hizo zimekuwa nguvu inayoendesha mabadiliko chanya katika mfumo wa elimu, ukigusa maisha ya wengi.

Kwa upande wake, Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mhe. Charlotta Ozaki Marcias, alisema kuwa tangu Tanzania ijiunge na Taasisi ya Ushirikiano wa Elimu Duniani (Global Partneship for Education-GPE), mwaka 2013, sekta ya elimu imeboreshwa ikiwemo kupungua kwa msongamano wa wanafunzi wa shule za msingi madarasani kutoka wastani wa wanafunzi 113 hadi kufikia wanafunzi 50.

Alisema kuwa Serikali yake itaendelea kutimiza wajibu wake wa kuwa wakala wa kutafuta fedha kwa ajili ya kuiwezesha Serikali kutimiza wajibu wa kuboresha mifumo ya elimu nchini.



Utekelezaji Miradi >




# Rais mstaafu Dkt. Kikwete na Afisa Mtendaji Mkuu GPE wakoshwa na utekelezaji miradi

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE), Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Afisa Mtendaji Mkuu wa GPE Laura Frigenti, watembelea na kukagua shule ya Msingi ya Maji Matitu iliyopo Mbagala na shule ya Mikongeni iliyopo Gongo la Mboto jijini Dar es salaam.

Katika ziara hiyo iliyofanyika siku tatu kabla ya mkutano wa Bodi ya GPE uliofanyika visiwani Zanzibar, Viongozi hao walijionea maendeleo ya miradi mbalimbali ambayo Shirika hilo limefadhili ikiwemo ujenzi wa Madarasa, Vyoo na Mafunzo endelevu ya Walimu kazini na kueleza kuridhishwa na utekelezaji.

Kwa upande wa shule ya Maji Matitu Shirika hilo limefadhili ujenzi wa madarasa nane na matundu 20 ya vyoo, wakati katika shule ya Mikongeni imechangia ujenzi wa madarasa mawili na matundu sita ya vyoo.

Dkt. Kikwete ameishukuru serikali ya Tanzania kwa kuendelea kushirikiana na GPE katika kuboresha sekta ya elimu hususan elimu kwa wasichana na kuahidi kuendelea kuunga mkono juhudi na mikakati ya kuiendeleza sekta hiyo.

Alisema Shirika hilo hadi sasa limeishaipatia Tanzania jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 332 takriban shilingi 834,980,332,000.00 ili kusaidia sekta ya elimu Tanzania Bara na Visiwani.

Kwa upande wake Afisa Mtendaji Mkuu wa GPE Bi. Frigenti aliipongeza serikali ya Tanzania kwa kujenga miundombinu bora na kuhakikisha kila mtoto anapatiwa haki ya elimu, huku akiwataka wadau wa maendeleo kuendelea kusaidia nchi zenye uhitaji, akisisitiza kwamba changamoto nyingi za kimaisha zinaweza kuepukika endapo wananchi watapatiwa elimu bora.

Frigenti alieleza kuridhishwa na matumizi ya Fedha ambayo GPE imekuwa ikitoa kwa Tanzania na kuahidi kuendeleza uhusiano mzuri uliopo na uliodumu kwa miaka 10 sasa.

Katika ziara hiyo Viongozi hao waliambatana na Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia Mhe. Omar Kipanga na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Deogratius Ndejembi pamoja na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Franklin Rwezimula.

Kwa niaba ya Serikali Viongozi hao wameishukuru GPE kwa kufadhili miradi ya elimu na kipekee kumshukuru Mhe. Kikwete kwa kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kutafuta rasilimali za kuimarisha Sekta ya Elimu.

Mitaala na Masomo ya Dini >



# Masomo ya Dini ni ya kipekee, ni tofauti na mitaala ya masomo mengine

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amebainisha kuwa, somo la dini na mitaala yake ni ya tofauti na ile ya masomo mengine kwani elimu hiyo inahusisha masuala ya imani na hugusa zaidi hisia.

Prof. Mkenda alisema hayo wakati akizindua Taasisi ya Tanzania Islamic Studies Teaching Association (TISTA) pamoja na kupokea muhtasari na kitabu cha kwanza cha mwanafunzi cha Elimu ya Dini ya Kiislamu, tukio lililofanyika katika ukumbi wa Mfalme Mohamed, BAKWATA makao makuu Jijini Dar es Salaam.

"Mitaala ya dini ni ya kipekee, ni tofauti na mitaala ya mfano somo la chemistry ambayo unaweza kuchukua Wataalamu wa chemistry popote ukaangalia na wa nchi nyingine ukaitengeneza, tofauti na ya dini inayovuta hisia na ikatokea tafsiri ambayo si sahihi inaweza kuibuka hisia kali sana". Amesema Prof. Mkenda.

Amesisitiza kuwa, katika hatua za kutekeleza kazi ya mabadiliko ya mitaala Serikali iliona upo umuhimu wa kuwashirikisha dini zote katika eneo la somo la Dini ili kushiriki kuandaa mitaala itayokuwa na maudhui sahihi na yenye manufaa kwa wanafunzi na bila kuadhiri maana.

Aidha, Prof. Mkenda amemshukuru Mufti wa Tanzania Shekh Abubakar Zuberi na Mufti wa Zanzibar na timu zake zote kutoka bara na zanzibar kwa ushirikiano anaoendelea kuuonesha katika kusimamia na maandalizi ya mtaala huo wa somo la Dini ya Kiislamu na kwa kutoa mapendekezo ambayo Serikali itayafanyia kazi.

Prof. Mkenda amesisitiza kuwa hakuna wakati ambapo Serikali ilitaka kuchukua kazi ya kuandaa Mitaala ya Masomo ya Dini kutokana na upekee wake na hivyo kuomba kuendelea na ushirikiano katika kuitekeleza mitaala hilo kwa ufanisi.

Sambamba na hilo, Prof. Mkenda amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kusisitiza kufanya mabadiliko ya wa mitaala ili kuandaa wahitimu wenye ujuzi na umahiri kulingana na uhitaji wa soko kitaifa na kimataifa.

Nae, Mufti Mkuu wa Tanzania Shekh Abubakar Zuberi amesema, uandaaji wa mtaala huo umeshirikisha umma wa Waislamu wote kutoka Tanzania na Zanzibar hivyo kuufanya muhtasari huo kubeba taswira ya michango, mawazo ya waislamu wote nchini.

Vile vile, aliishukuru Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi ya Elimu Tanzania kwa uongozi sahihi ya uliofanyika wa kuweka masomo ya dini katika mtaala huo mpya unaotarajia kuanza kutekelezwa kuanzia Januari 2024.

Changamoto za Walimu >

# Walimu ndio elimu, tuwasikilize ili kuzijua changamoto zao - Dkt Mtahabwa

Kamishna wa Elimu Tanzania Dkt. Lyabwene Mtahabwa ametoa wito kwa Wathibiti ubora wa shule na Maafisa Elimu Kata kuwaheshimu walimu na kuwasikiliza ili kufahamu Changamoto zao hali itayosaidia kuboresha Sekta ya elimu nchini.

Dkt. Mtahabwa ametoa rai hiyo Disemba 30, 2023 mkoani Morogoro wakati akifungua mafunzo ya mtaala ulioboreshwa kwa Wathibiti Ubora wa shule na Maafisa Elimu Kata, mtaala ulioanza kutekelezwa kuanzia Januari 2024.

"Elimu katika nchi yoyote ile ni mwalimu, ukijua hilo jifunze kufanya kazi vizuri na mwalimu, jifunze kumheshimu, kumpenda, kumthamini tusitoe maelekezo bila kuwapa elimu ya jambo lolote, naomba tutumie nafasi zetu vizuri na kuongea nao kwa staha." Alisema Dkt. Mtahabwa.

Alieleza kuwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 Toleo la 2023, inasisitiza kuinua hadhi ya elimu, hivyo amewataka Wataalamu hao kuwa wanyenyekevu kwa walimu wanaowaongoza ili kuwasaidia kuleta matokeo chanya katika Sekta ya Elimu nchini.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Msingi na Elimu ya Awali kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Bi. Suzanne Nusu amesema, kama watekelezaji wa Sera watahakikisha wanatoa ushirikiano kwa Wizara ya Elimu na Taasisi ya Elimu ili Mtaala huu ulioboreshwa unaenda kuwa chachu ya mabadiliko katika Sekta ya Elimu.

Nae, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Elimu Tanzania Dkt. Aneth Komba ametoa wito kwa Wathibiti ubora wa shule kuzingatia kwa undani mafunzo hayo yanayotolewa na TET ili kwenda kuwafundisha walimu wote kwenye Kata zao kuuelewa mtaala mpya na namna bora ya kuutekeleza.

Amesema, Maafisa Elimu kata na Wathibiti ubora wa shule ni wawakilishi wa TET katika maeneo yao ya utendaji hivyo ni muhimu kusaidia kutatua changamoto zinazowakumba walimu katika shule zao badala ya kuandika taarifa ya changamoto hizo bila kusaidia katika utatuzi.

Aidha, Dkt. Komba amesema, Taasisi ya Elimu Tanzania itaendelea kushirikiana na Maafisa Elimu Kata pamoja na Wathibiti ubora wa shule ili kuhakikisha ubora wa elimu unatekelezwa katika ngazi zote ikiwemo kupitia mitaala iliyoboreshwa pamoja na upatikanaji wa vitabu.



Maelekezo VETA >



# Kipanga ahimiza ujenzi wa VETA Arumeru



Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Mhe. Omari Kipanga amewahimiza Wasimamizi wa mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Ufundi VETA Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha kukamilisha hatua ya kwanza ya kujenga msingi kwa wakati na kuwataka kufanya marekebisho katika maeneo yenye Changamoto alizobaini wakati wa ziara yake.

Mhe. Kipanga ametoa rai hiyo akiwa katika ziara ya Kukagua na kufanya tathmini ya ujenzi wa Chuo hicho ikiwa ni moja ya VETA 63 zinazojengwa na Serikali nchini.

Katika hatua nyingine Naibu Waziri Kipanga amemtaka Mhandisi na Mshauri Elekezi kuwepo eneo la ujenzi wakati wote ili kuhakikisha mafundi wanajenga kwa ufanisi na kufuata taratibu zote za ujenzi.

Aidha amehimiza umakini kwa mafundi wanaojenga karakana na madarasa ya Chuo hicho kufuata maelekezo yote wanayopewa na Wahandisi sambamba na vipimo na michoro iliyopo kwenye ramani za ujenzi.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Halmashauri ya wilaya ya Arumeru Jeremia Kashiri ameishukuru Serikali kwa kutenga fedha za Ujenzi wa chuo hicho cha wilaya na kumshukuru Naibu Waziri huyo kwa kufanya ukaguzi, tathmini na kushauri.

Maendeleo Vyuo Vikuu >

# Mabaraza ya wahitimu chachu ya maendeleo vyuo vikuu - Prof. Mkenda

Waziri wa Elimu, Sayansi na teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema serikali inatambua umuhimu wa Mabaraza ya Wahitimu na Jumuiya mbalimbali katika Vyuo Vikuu, katika kuchangia Maendeleo ya miradi mbalimbali katika Vyuo husika.

Waziri Mkenda alitoa kauli hiyo mjini Morogoro wakati akihutubia Baraza la Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe ambapo amesema serikali inajivunia michango ya Wajumbe wa Baraza hilo, ikiwemo mchango wa ujenzi wa mabweni kwa ajili ya Wanafunzi Ndaki ya Mbeya.

"Lakini pia nawapongeza kufikia katika hatua za mwisho za kuanzisha mfuko wa ufadhili kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wasio na uwezo kugharamia masomo, na kwamba Sera ya mfuko huo tayari imeandaliwa na kupitishwa na ngazi husika nawapongeza sana na ninaamini katika utoaji ufadhili mtazingatia pia meritocracy" alisema Prof. Mkenda.

Nae Rais wa Baraza la Wahitimu katika Chuo Kikuu Mzumbe CPA. Ludovick Utoah ameipongeza serikali kwa kuendelea kusimamia mageuzi makubwa yenye mchango chanya katika sekta ya elimu kwa kuzingatia viwango vya juu.

Mkuu wa mkoa wa Morogoro Mhe. Adam Malima amemshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kuendelea kufanya uwekezaji kwa kuboresha mbiundombinu ya elimu katika Vyuo Vikuu ikiwemo Chuo Kikuu cha Mzumbe ambacho kimekuwa kinara katika kuzalisha Wataalam katika masuala ya uongozi.

Akitoa taarifa kuhusu utekelezaji wa miradi na shughuli mbalimbali za kitaaluma Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe Prof. William Mwegoha amesema Chuo hicho kinaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuhuisha mitaala iweze kuakisi mabadiliko makubwa yanayotarajiwa katika taifa hilo.

"Tunatambua mageuzi haya yanaakisi malengo ya serikali ya awamu ya Sita ambayo inasisita umuhimu wa elimu inayotolewa katika ngazi zote nchini, kukidhi mahitaji ya jamii katika taifa letu" alisema Prof. Mwegoha.



## NUKUU > TUTAJIELEKEZA KATIKA KUFANYA MAPITIO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014 NA KUFANYA MAREKEBISHO KWENYE MITAALA ILIYOPO ILI IELEKEZWE KWENYE KUTOA ELIMU UJUZI KULINGANA NA MAZINGIRA YA NCHI NA SOKO LA AJIRA

***– Mhe. Samia Suluhu Hassan,***
***Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania***
***Bungeni - April, 2021***

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P. 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz